# JARIDA LA WAKILI MKUU

ISSN 2686 - 2686 | Toleo Na. 16 | Disemba, 2025 - Machi, 2026



# Bodi ya Uhariri

## Mwenyekiti

**Alice E. Mtulo**
Naibu Wakili Mkuu wa Serikali

## Mhariri Mkuu

**Prisca J. Ulomi**
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

## Waandishi wa Jarida

**Prisca J. Ulomi**
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

**Dennis J. Buyekwa**
Afisa Habari

## Msanifu wa Jarida

**Nyamhoni R. Chacha**
Afisa TEHAMA

## Wajumbe

**Saddy R. Sevingi**
Mkurugenzi wa Usuluhishi

**ACPA Devota M. Ngulugulu**
Mhasibu Mkuu

**Mercy R. Kyamba**
Mkurugenzi Msaidizi - Udhibiti Ubora

**Kiuye M. Shemakame**
Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Maktaba na Utafiti

**Stanley S. Kalokola**
Wakili wa Serikali Mwandamizi

**Zuhura M. Kussaga**
Mchumi Mwandamizi

# Tahariri ya Mhariri



**Prisca Jackson Ulomi**
**Mhariri Mkuu**

Awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kukutana tena kupitia Jarida hili ambalo linaendelea kuwa jukwaa muhimu la kuhabarisha umma na wadau kuhusu majukumu, mafanikio na shughuli za Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ambapo kupitia makala na uchambuzi wa taarifa mbalimbali, jarida limeendelea kuweka kumbukumbu muhimu za kitaasisi ambazo zimesaidia kuongeza uelewa wa jamii kuhusu mchango wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika uendeshaji wa mashauri ya Serikali na kuendelea kulinda maslahi ya Taifa.

Aidha, miongoni mwa masuala yaliyopewa kipaumbele kipindi hiki ni ziara ya kikazi ya Wakili Mkuu wa Serikali alipomtembelea Rais wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu. Ziara ambayo ina umuhimu mkubwa katika kuimarisha ushirikiano wa taasisi za kisheria katika ngazi ya kikanda na kimataifa. Ushirikiano huu umesaidia kwa kiasi kikubwa kubadilishana uzoefu, kujenga uelewa wa pamoja kuhusu masuala ya sheria za haki za binadamu na kuboresha usimamizi wa mashauri yanayohusisha Serikali.

Sambamba na hilo, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeendelea kuwekeza katika rasilimali watu kwa kuendesha mafunzo kwa waajiriwa wapya. Mafunzo haya ni hatua muhimu katika kuwajengea watumishi wapya uwezo na uelewa wa majukumu ya taasisi, maadili ya utumishi wa umma pamoja na mbinu bora za utendaji katika utekelezaji wa majukumu ya Serikali.

Kupitia mafunzo hayo, watumishi wanapata msingi imara wa kitaaluma unaowawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi, weledi na uwajibikaji. Hatua hii inaendana na dhamira ya OWMS kuendelea kujenga wataalamu wenye uwezo wa kulinda maslahi ya Serikali katika kusimamia mashauri kwenye mahakama na mabaraza ya usuluhishi ndani na nje ya nchi.

Vilevile, uendeshaji wa mikutano ya Baraza la Wafanyakazi umeendelea kuwa nyenzo muhimu katika kuimarisha ushirikiano na mawasiliano kati ya menejimenti na watumishi wa OWMS, ambapo kupitia vikao hivi, masuala mbalimbali yanayohusu ustawi wa watumishi, mazingira ya kazi na utekelezaji wa majukumu ya taasisi hujadiliwa kwa uwazi na kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi, mikutano hii pia hutoa fursa kwa watumishi kushiriki katika maamuzi yanayohusu taasisi, hali inayochangia kujenga ari ya kazi, uwajibikaji na mshikamano ndani ya Ofisi.

Mwisho, tunawahimiza wadau na wasomaji kuendelea kufuatilia machapisho ya jarida hili ili kupata taarifa sahihi kuhusu maendeleo na shughuli za taasisi hii muhimu katika mfumo wa utawala wa sheria nchini.



# Dawati la Mwenyekiti

**Alice E. Mtulo**
**Naibu Wakili Mkuu wa Serikali**

Toleo la Kumi na Sita la Jarida la Wakili Mkuu limeangazia mambo muhimu yaliyotekelezwa katika kipindi cha mwezi Desemba, 2025 hadi Machi, 2026.

Jarida hili limeangazia mafanikio ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ikiwemo taarifa ya mafanikio ya Siku 100 za kipindi cha awamu ya pili ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Katika kipindi cha Siku 100 za Serikali ya Awamu ya Sita, OWMS imetekeleza majukumu yake kwa weledi na ufanisi zaidi kwa kuiwakilisha vyema Serikali katika uratibu, usimamizi na uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi yaliyofunguliwa na au dhidi ya Serikali na taasisi zake ndani na nje ya nchi.

Hatua hizi zimechangia kulinda rasilimali za umma na kuhakikisha maslahi ya Taifa yanalindwa ipasavyo.

Katika kuimarisha miundombinu ya taasisi, ziara ya Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa jengo la OWMS katika Mji wa Serikali Mtumba, jijini Dodoma imeripotiwa kwenye toleo hili ikianisha hatua za maendeleo ya ujenzi.

Aidha, OWMS imeendelea kuimarisha ushirikiano na taasisi mbalimbali za Serikali pamoja na wadau wa Sekta ya Sheria ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Hususan, OWMS imeshirikiana na kituo cha kimataifa cha usuluhishi cha Tanzania (TIAC) katika kutoa mafunzo na kuwajengea uwezo wanawake kushiriki kwenye utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi.

Vilevile katika kipindi hiki pia, Ofisi imeendelea kuboresha mifumo ya utendaji kazi kwa kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ikiwemo mfumo wa usimamizi wa mashauri na maktaba mtandao. Mifumo hii imechangia kuongeza uwazi, uwajibikaji na ufanisi katika utoaji wa huduma za kisheria.

Mafanikio haya yanaakisi dhamira ya dhati ya OWMS, katika kuunga mkono juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuimarisha utawala bora, unaotumia mifumo ya kisasa katika usimamizi wa shughuli za umma na kurahisha utoaji haki kwa wakati ili kulinda rasilimali za Taifa.

Haya ni baadhi ya masuala machache yatakayoakisiwa ndani ya Jarida hili.

Nitumie nafasi hii kuomba wasomaji wetu kuendelea kutoa maoni kwa Bodi ya Uhariri wa Jarida la Wakili Mkuu kwa lengo la kuboresha Jarida hili. Kwa pamoja tutaweza kulifanya Jarida kuendelea kutoa mchango chanya katika ukuaji wa Sekta ya Sheria hapa nchini.

Nawatakia usomaji mwema wa Toleo la kumi na Sita la Jarida la Wakili Mkuu.

Asanteni.

# Yaliyomo

Uk. 06 - Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Yaokoa Shilingi Bilioni 826.6

Uk. 07 - Dkt. Nchimbi Aitaka Mahakama Kuendelea Kuwa Nguzo ya Utoaji Haki Nchini

Uk. 09 - Waziri Homera Aipa Kongole OWMS kwa Utendaji Kazi kwa Weledi

Uk. 13 - Wakili Mkuu wa Serikali Akutana na Rais wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu

Uk. 16 - Wakili Mkuu wa Serikali Ashiriki Ufunguzi wa Mwaka wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu

Uk. 20 - OWMS Yajipanga Uendeshaji wa Majukumu ya Kisheria

Uk. 23 - SG Akagua Ujenzi wa Jengo la Ofisi Mtumba, Dodoma

Uk. 26 - Mpango Mkakati wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Kufikia Dira 2050

Uk. 28 - Dkt. Possi: Viongozi ni Taswira ya Taasisi na Serikali kwa Jamii

Uk. 32 - Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi Ampongeza Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Uk. 34 - OWMS Yawasilisha Taarifa ya Utekelezaji kwa Kamati ya Bunge

Uk. 37 - Kliniki za Sheria Kutatua Kero za Wananchi Zenye Mfumo wa Sheria

Uk. 40 - Wakili Mfawidhi Mkoani Manyara Azitaka Mamlaka Kujiepusha na Utoaji wa Hati kwa Mwananchi Zaidi ya Mmoja.

Uk. 42 - Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo Awahimiza Watumishi wa OWMS Kufanya Kazi kwa Bidii

Uk. 46 - Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Yashiriki Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani

Uk. 50 - Habari Picha

Uk. 51 - Waajiriwa Wapya Wapewa Mafunzo ya Sheria, Taratibu na Kanuni za Utumishi wa Umma

Uk. 54 - Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Yashiriki Bonanza la Mahakama

Uk. 56 - Mahakama Yatupilia Mbali Shauri la Kupinga Tume ya Uchunguzi wa Matukio ya Uvunjifu wa Amani Baada ya Uchaguzi Mkuu wa Tarehe 29 Oktoba, 2025

Uk. 57 - OWMS Yashiriki Kuendesha Mafunzo, Kongamano la Ushirikishwaji wa Wanawake Kwenye Usuluhishi wa Migogoro kwa Njia Mbadala

Uk. 60 - Dira, Dhima na Maadili ya Msingi



# Siku 100

## za Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

# Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Yaokoa Shilingi Bilioni 826.6

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, imefanikiwa kuokoa shilingi bilioni 826.5 katika uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi. Hatua hii itasaidia Serikali kutekeleza miradi ya maendeleo kwa lengo la kuwaletea wananchi wake maendeleo.

Hayo yamesemwa na Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice E. Mtulo wakati akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya OWMS ndani ya siku 100 za kipindi cha pili cha Serikali ya Awamu ya Sita kwa Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Juma Homera (Mb).

Bi. Mtulo alieleza kuwa kiasi cha fedha kilichookolewa baada ya Serikali kumaliza mashauri matatu (03) ya usuluhishi kwa njia ya majadiliano. Kati ya mashauri hayo, mashauri mawili (02) yalihusu usuluhishi wa kitaifa na shauri moja (01) ni la usuluhishi wa kimataifa.

Kiasi kilichokolewa ni fedha ambazo Serikali ingelipa endapo ingeshindwa katika uendeshaji wa mashauri hayo. Fedha zilizookolewa zitaelekezwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.
Akizungumzia uendeshaji wa mashauri ya madai, Bi. Mtulo alisema kuwa OWMS imemaliza jumla ya mashauri 97 na kuokoa kiasi cha Shilingi 3,151,253,696.46 kwa mashauri yaliyohusisha fedha.

Alifafanua kuwa mashauri 75 yaliyofunguliwa kupinga matokeo ya Uchaguzi Mkuu uliofanyika mwezi Oktoba, 2025 ambapo mashauri 33 ni ya Zanzibar na mashauri 42 ni ya Tanzania Bara. Mpaka sasa mashauri 35 kati ya 75 yamemalizika kwa Serikali kushinda na kuokoa fedha ambazo zingetumika kurudia uchaguzi na gharama nyinginezo. Aidha, mashauri 40 yaliyobaki yanaendelea katika hatua mbalimbali.

Bi. Mtulo aliendelea kufafanua kuwa, OWMS imeshinda Shauri la Rufaa Na. 4 ya mwaka 2023 lililofunguliwa kupinga ujenzi wa bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani Tanga, katika Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki. Shauri hilo lilifunguliwa na Asasi za Kiraia zikiongozwa na Centre for Food and Adequate Living Rights (CEFROHT) dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Uganda, Tanzania na Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hatua hii imesaidia kuchochea shughuli za maendeleo ya wananchi kwa nchi zote mbili za Tanzania na Uganda.






*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi akizungumza kwenye Maadhimisho ya Siku ya Sheria yaliyofanyika tarehe 02 Februari, 2026 Makao Makuu ya Mahakama ya Tanzania jijini Dodoma.*

# Dkt. Nchimbi Aitaka Mahakama Kuendelea Kuwa Nguzo ya Utoaji Haki Nchini

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi, akimwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan katika Maadhimisho ya Siku ya Sheria nchini. Maadhimisho hayo yalifanyika kitaifa katika viwanja vya Mahakama, jijini Dodoma tarehe 2 Februari, 2026.

Maadhimisho ya Siku ya Sheria nchini kwa mwaka 2026 yalibeba kauli mbiu isemayo, "***Mchango wa Mahakama katika Ustawi wa Maendeleo ya Taifa***".

Awali, akitoa salamu za Mhe. Rais, Mhe. Balozi Dkt. Nchimbi alimshukuru Jaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania, Mhe. George Masaju kwa kumualika Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa mgeni rasmi katika Maadhimisho hayo.

Mhe. Balozi Dkt. Nchimbi amesisitiza dhamira ya Serikali katika kuhakikisha kuwa mhimili wa Mahakama unaendelea kutoa haki kwa wananchi na kuwa nguzo muhimu ya ustawi wa jamii, maendeleo ya kiuchumi na ustawishaji wa amani ya Taifa.

*"Mahakama ndio mhimili unaohakikisha kuwa haki inapatikana kwa wote bila upendeleo, hofu wala uonevu wa aina yoyote,"* amesema Mhe. Balozi Dkt. Nchimbi.

Aidha, Mhe. Balozi Dkt. Nchimbi amesema kuwa Serikali itaendelea kushirikiana na Mahakama katika ujenzi wa miundombinu, kuimarisha rasilimali watu na kusogeza huduma za utoaji haki karibu zaidi na wananchi.

Jaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania, Mhe. George Masaju amesema kuwa Mahakama itaendelea kutoa haki kwa wananchi ili kuhakikisha kuwa inachangia ustawi na maendeleo ya wananchi na taifa kwa ujumla.

*"Uwepo wa haki katika maamuzi ya Mahakama, kunachangia amani na udugu baina ya wananchi na hivyo kuwawezesha kuendelea kufanya shughuli zao za kijamii, kiuchumi na kisiasa kwa ufanisi,"* alisema Mhe. Masaju.

Awali, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Samwel Maneno akimwakilisha Mwanasheria Mkuu wa Serikali, amesema kuwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itaendelea kushirikiana na Mahakama ya Tanzania ili kuhakikisha wananchi wanaendelea kupata huduma za kisheria na upatikanaji wa haki kwa urahisi zaidi.

Aidha, Mhe. Maneno alieleza kuwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa Sekta ya Sheria imeanza kufanya maboresho ya sheria, sera, mipango, malengo na mikakati mbalimbali. Hatua hii ni pamoja na kufanya tafiti za kitaalamu ili kuhakikisha kuwa masuala yote yanayohusu tasnia ya sheria yanafungamanishwa na Dira 2050.




*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi akiwa kwenye picha ya pamoja na viongozi mbalimbali akiwemo Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi (aliyesimama nyuma katikati) wakati wa maadhimisho ya Siku ya Sheria yaliyofanyika jijini Dodoma.*




# Waziri Homera Aipa Kongole OWMS kwa Utendaji Kazi kwa Weledi

Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Juma Homera (Mb), ameipongeza Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa utendaji kazi kwa weledi katika usimamizi na uendeshaji wa mashauri ya madai, katiba, haki za binadamu na usuluhishi kwa niaba ya Serikali na taasisi zake ndani na nje ya nchi.

Mhe. Dkt. Homera ameyasema hayo alipofanya ziara yake ya kwanza OWMS baada ya kuteuliwa kuongoza Wizara hiyo kwa lengo la kujitambulisha, kufahamiana na mejimenti ya OWMS na kufahamu majukumu ya Ofisi hiyo.

*"Hongereni kwa kazi kubwa, muendelee kuifanya kwa weledi, uzalendo, nasi Wizarani tutaendelea kuwapa ushirikiano ili muweze kutekeleza majukumu yenu kwa ufanisi zaidi na tutangulize maslahi ya taifa mbele,"* alisisitiza Mhe. Dkt. Homera.

Katika ziara hiyo, Mhe. Waziri Dkt. Homera aliambatana na Naibu Waziri, Mhe. Zainab Katimba.

Mhe. Dkt. Homera aliwasihi wajumbe wa menejimenti na watumishi kuwa waendelee kutumia mifumo ya TEHAMA katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku.

Mifumo hii inahitajika katika Sekta ya Sheria ikiwa ni pamoja na kutekeleza azma ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha kuwa Serikali inatumia mifumo ya TEHAMA na inasomana.

Naye Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi alisema kuwa OWMS ni lango la uchumi na maslahi ya taifa. Hivyo, OWMS itaendesha mashauri ya madai na usuluhishi kwa niaba ya Serikali na taasisi zake kwa kuhakikisha kuwa maslahi mapana ya taifa yanalindwa.

Akiwasilisha taarifa ya OWMS kwa niaba ya menejimenti, Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice E. Mtulo aliwaarifu viongozi hao kuwa OWMS imeendesha jumla ya mashauri 10,576 ya madai na kati ya hayo imemaliza mashauri 1,715. Pia, imeendesha mashauri 258 ya usuluhishi na imemaliza mashauri 35 kati ya hayo hadi kufikia mwezi Desemba, 2025.

Pia, Bi. Mtulo aliongeza kuwa OWMS inakwenda sambamba na maelekezo ya Serikali ambapo tayari inatumia Mfumo wa Usimamizi na Uendeshaji wa Mashauri (*Case Information Management System - CIMS)* kupokea, kusajili, kupanga, kupata takwimu sahihi za mashauri na kwa wakati na kutunza taarifa na idadi za mwenendo wa mashauri hayo.

Kikao hicho kilihudhuriwa na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dkt. Franklin Rwezimula aliyemwakilisha Katibu Mkuu, ndugu Eliakim Maswi, baadhi ya watumishi kutoka Wizara hiyo, wajumbe wa menejimenti na watumishi wa OWMS.



*Viongozi na baadhi ya Watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, wakimsikiliza Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Dkt. Juma Homera (hayupo pichani) wakati akizungumza nao kwenye ukumbi wa mikutano wa Ofisi hiyo Jijini Dar es Salaam.*




*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi akizungumza kwa niaba ya Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakati wa ziara ya Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Juma Homera (hayupo pichani) alipotembelea ofisi hiyo Jijini Dar es Salaam.*




*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakati wa ziara ya Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Juma Homera (Mb) alipotembelea Ofisi hiyo jijini Dar es Salaam.*



*Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Zainab Katimba akitoa salamu za Wizara kwa watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakati wa ziara ya Waziri alipotembelea Ofisi hiyo jijini Dar es Salaam.*

*Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, Dkt. Franklin Rwezimula akimkaribisha Naibu Waziri kuzungumza na Watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakati wa ziara yao walipotembelea Ofisi hiyo jijini Dar es Salaam.*






*Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Juma Homera (Mb) akipokea jarida, nyaraka na kadi ya pongezi kutoka kwa Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi (aliyesimama katikati) alipotembelea Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Jijini Dar es Salaam. Anayeshuhudia ni Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo.*




*Dkt. Ally Possi, Wakili Mkuu wa Serikali (aliyeketi kushoto) akizungumza na Mhe. Jaji Blaise Tchikaya, Rais wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu alipotembelea Mahakama hiyo kwa lengo la kujitambulisha na kujadiliana kuendeleza ushirikiano baina ya Ofisi hizo walipokutana kwenye Mahakama hiyo jijini Arusha.*

# Wakili Mkuu wa Serikali Akutana na Rais wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu

Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi amekutana na Rais wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, Mhe. Jaji Blaise Tchikaya na kufanya mazungumzo nae Ofisi kwake jijini Arusha kwa lengo la kujitambulisha ili kuendeleza ushirikiano uliopo baina ya Ofisi hizo mbili.

Dkt. Possi alisema kuwa Tanzania kama nchi mwenyeji na kwa kuzingatia majukumu ya OWMS ameona ni muhimu kufika, kujitambulisha na kumpongeza kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Mahakama hiyo.

*"OWMS ina jukumu la kuendesha mashauri ya haki za binadamu na watu kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Utakutana na Ofisi hii mara kwa mara katika kuendesha mashauri hayo. Hivyo,*

*nimeona nifike tuzungumze ili kukuhakikishia ushirikiano na Ofisi hii kwa niaba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika uendeshaji wa mashauri kwenye Mahakama hii,”* alisisitiza Dkt. Possi.

Pia, Dkt. Possi aliongeza kuwa yuko tayari kupokea ujumbe wa Mahakama kwa niaba ya Serikali ili kuweza kuwasilisha kwa kuwa Ofisi imekuwa inashirikiana na Mahakama hii katika muktadha huo.

Naye Mhe. Jaji Tchikaya, alisema mashauri mengi yanayoendeshwa na Mahakama hiyo yanatokea Tanzania. Hii inaonesha kuwa uwepo wa Mahakama hii Tanzania, inawapa fursa wadau kuitumia baada ya kupita kwenye Mahakama za ndani.

Mhe. Jaji Tchikaya aliongeza kuwa hii inaonesha Tanzania inaruhusu wananchi wake kutafuta na kupata haki kupitia vyombo vya kimataifa ikiwemo Mahakama hii. Jambo hili ni ushahidi wa utekelezaji wa Mkataba na Itifaki ya Haki za Binadamu na Watu ya Umoja wa Afrika.

Katika hatua nyingine, Mhe. Jaji Tchikaya ameomba ushirikiano wa Dkt. Possi katika kuongeza msukumo wa ujenzi wa Ofisi ya Mahakama hiyo ili uweze kukamilika. Pia, aliishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kufanikisha kuanza kwa ujenzi wa Ofisi ya Mahakama hiyo jijini Arusha.



*Mawakili wa Serikali wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakimsikiliza Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi (hayupo pichani) wakati akizungumza na Mhe. Jaji Blaise Tchikaya, Rais wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu alipotembelea Mahakama hiyo jijini Arusha.*




*Dkt. Ally Possi, Wakili Mkuu wa Serikali (kushoto) akimkabidhi Jarida ya Wakili Mkuu, Rais wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, Mhe. Jaji Blaise Tchikaya alipotembelea Mahakama hiyo kwa lengo la kujitambulisha jijini Arusha.*




*Dkt. Ally Possi, Wakili Mkuu wa Serikali (aliyesimama katikati) akiwa kwenye picha ya pamoja na baadhi ya watumishi wa OWMS baada ya kutembelea Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu jijini Arusha.*

# Rais wa Jamhuri ya Ghana Afungua Mwaka wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu

## Wakili Mkuu wa Serikali Ashiriki Ufunguzi




*Mhe. John Dramani Mahama, Rais wa Jamhuri ya Ghana akizungumza na viongozi na wadau wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu wakati akifungua Mwaka wa Mahakama hiyo Jijini Arusha.*

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilishiriki ufunguzi wa Mwaka wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu mwaka 2026 na uzinduzi wa maadhimisho ya miaka 20 ya Mahakama hiyo.

Maadhimisho hayo yalibeba kauli mbiu isemayo, ***"Miaka 20 ya Utumishi katika Kulinda Haki za Binadamu na Watu"***.

Ufunguzi huo ulifanyika kwenye ukumbi wa Mahakama hiyo jijini Arusha na ulifunguliwa rasmi na Mhe. John Dramani Mahama, Rais wa Jamhuri ya Ghana na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wa Serikali za nchi za Afrika, wadau wa maendeleo, mabalozi, wawakilishi wa Umoja wa

Mataifa wanaoshughulikia masuala ya haki za binadamu na wadau wa Sekta ya Sheria wa ndani na nje ya Tanzania.

Mhe. Mahama wakati akifungua rasmi mwaka wa Mahakama hiyo alisema Mahakama inalinda haki zetu. Hivyo, tuiwezeshe Mahakama katika kusimamia ulinzi wa haki za binadamu na utu wa watu.

*"Kila mmoja katika Bara la Afrika awe mlinzi wa amani, na ndoto za waanzilishi wa mataifa yetu ili miaka 20 ijayo Mahakama hii iwe chombo cha mfano katika kulinda haki za binadamu duniani,"* alisisitiza Mhe. Rais Mahama.

Kwa upande wa Tanzania, Mhe. Zainab Katimba, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria alimwakilisha Waziri, Mhe. Dkt. Juma Homera ambapo alisema kuwa anaipongeza Mahakama ya Afrika kwa kuboresha utendaji kazi wake kwa kusimamia na kuhakikisha haki inapatikana kwa wananchi wa Afrika.

Mhe. Katimba aliongeza kuwa Tanzania imeendelea kuzingatia na kuimarisha utawala wa sheria na haki za binadamu ili haki itendeke kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

Naye Rais wa Mahakama hiyo, Mhe. Jaji Blaise Tchikaya alisema ni muhimu kwa nchi wanachama kuwa na umiliki wa pamoja wa maamuzi ya Mahakama katika uzingatiaji




***Dkt. Ally Possi, Wakili Mkuu wa Serikali (wa kwanza kulia) akimsikiliza Rais wa Ghana, Mhe. John Dramani Mahama wakati akifungua Mwaka wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu Jijini Arusha.***

wa haki za binadamu. Pia, aliongeza kuwa hadi kufikia mwezi Februari, 2026 Mahakama hiyo ilipokea maombi 390 ya masuala mbalimbali ya haki za binadamu na kutekeleza majukumu yake. Maombi hayo yanahusu mashauri ya uchaguzi, uhuru wa kujieleza, uhuru wa kukusanyika, ulinzi wa makundi ya pembezoni, haki za wanawake na mabinti, ulipaji fidia, haki za watoto na ustawi wao.

Naye Dkt. Ally Possi, Wakili Mkuu wa Serikali alisema OWMS imeshiriki ufunguzi wa mwaka wa Mahakama ya Afrika na maadhimisho ya miaka 20 ya Mahakama kwa lengo la kuimarisha ushirikiano, umoja na

mshikamano baina ya OWMS na Mahakama hiyo.

*“Tanzania ni mwenyeji wa Mahakama hii na tumeitunza kwa miaka 20 hadi sasa. OWMS imekuwa ikiendesha mashauri mbalimbali yanayohusu haki za binadamu yanayoikabili Tanzania katika Mahakama hii. Aidha, Ofisi imekuwa mdau muhimu katika kushiriki mafunzo na matukio mbalimbali ya Mahakama. Hivyo, tumeona umuhimu wa kushiriki ufunguzi huu ili tuendeleze ushirikiano uliopo baina ya Ofisi na Mahakama katika uendeshaji wa mashauri ya mwaka huu,”* alifafanua Dkt. Possi.

Tukio hilo lilihudhuriwa na viongozi mbalimbali waliotoa salamu kutoka kwenye makundi yao ikiwa ni pamoja na Mhe. Balozi Selma Malika Haddadi, Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Umoja wa Afrika, Mhe. Willy Nyamitwe, Balozi wa Jamhuri ya Burundi katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Shirikisho la Ethiopia, Mhe. Idrissa Sow, Mwenyekiti, Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, Mhe. Jaji Pascal Bamouni, Rais wa Mahakama ya Kadhi, Burkina Farso na mwakilishi wa Mahakama zinazoshiriki, ndugu Herve Kuate, Kamishna Mkuu wa Wakimbizi wa Umoja wa Mataifa (UNHCR) na Bi. Sophia Ebby, Mratibu wa Muungano wa Mahakama ya Afrika.




*Mhe. Jaji Blaise Tchikaya, Rais wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, akizungumza na viongozi na wadau wa Mahakama wakati wa ufunguzi wa Mwaka wa Mahakama hiyo Jijini Arusha.*



*Mawakili wa Serikali wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (waliovaa majoho) wakimsikiliza Mhe. Jaji Blaise Tchikaya, Rais wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (hayupo pichani) wakati wa ufunguzi wa Mwaka wa Mahakama hiyo Jijini Arusha.*



*Mhe. John Dramani Mahama, Rais wa Jamhuri ya Ghana (aliyeketi katikati) akiwa kwenye picha ya pamoja na viongozi na wadau wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu baada ya kufungua mwaka wa Mahakama hiyo Jijini Arusha.*




# OWMS Yajipanga Uendeshaji wa Majukumu ya Kisheria

## Menejimenti Yafanya Tathmini ya Utendaji Kazi

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali yafanya tathmini ya utendaji kazi katika kipindi cha nusu Mwaka wa Fedha 2025/26 na kujipanga kutekeleza majukumu yake katika kipindi cha mwezi Januari, 2026 hadi Juni, 2026.

Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi aliendesha kikao cha menejimenti cha kutathmini utendaji kazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kilichofanyika jijini Dodoma. Lengo la kikao hicho ni kuchambua taarifa ya utekelezaji na kupanga mikakati mipya ya utendaji kazi ili kuhakikisha Ofisi inaendesha mashauri ya madai na usuluhishi kwa tija na ufanisi.

*"Kikao hiki ni cha kimkakati, lengo ni kujipanga kuendesha majukumu ya kisheria ya Ofisi ikizingatiwa kuwa kikao hiki kinafanyika kuelekea Siku ya kilele cha Wiki ya Sheria inayoadhimishwa kila mwaka mwanzoni mwa mwezi Februari,"* alisisitiza Dkt. Possi.

Pia, Dkt. Possi aliongeza kuwa Ofisi imedhamiria kufungua Ofisi nyingine kwenye mikoa ya Katavi, Geita, Singida ili kusogeza huduma karibu na



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice E. Mtulo akifuatilia majadiliano ya kikao cha menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali cha kutathmini utendaji kazi wa Ofisi hiyo kilichofanyika jijini Dodoma.*

wananchi. Aidha, aliwataka wajumbe wa menejimenti ya Ofisi hiyo kuendelea kutumia mifumo ya TEHAMA katika utendaji kazi.

Naye Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice E. Mtulo akizungumza kwa niaba ya menejimenti ya OWMS alimhakikishia Dkt. Possi kuwa wajumbe wa menejimenti hiyo wataendelea kutekeleza majukumu kwa wakati katika kipindi cha pili cha Mwaka wa Fedha 2025/26.

Kikao hicho hufanyika mara moja kwa mwaka ili kuwapa muda wa kutosha wajumbe wa menejimenti ya OWMS kutoa taarifa ya utendaji kazi na majukumu yaliyopangwa kutekelezwa kwa kipindi cha pili cha Mwaka wa Fedha kwa mwaka husika.



*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi (aliyesimama katikati mbele) akiwa kwenye picha ya pamoja na Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice E. Mtulo (kulia kwake) kabla ya kikao cha menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali cha kutathmini utendaji kazi wa Ofisi hiyo kilichofanyika jijini Dodoma.*




*Baadhi ya wajumbe wa menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakimsikiliza Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi (hayupo pichani) wakati wa kikao cha menejimenti ya Ofisi hiyo cha kutathmini utendaji kazi kilichofanyika jijini Dodoma.*




*Baadhi ya wajumbe wa menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakimsikiliza Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi (hayupo pichani) wakati wa kikao cha menejimenti ya Ofisi hiyo cha kutathmini utendaji kazi kilichofanyika jijini Dodoma.*

# Wakili Mkuu wa Serikali Akagua Ujenzi wa Ofisi, Mtumba - Dodoma



*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi akizungumza na wajumbe wa Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Mkandarasi - Suma JKT na mshauri elekezi, TBA (hawapo pichani) wakati wa ziara yake ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa jengo la Ofisi hiyo unaoendelea katika Mji wa Serikali, Mtumba, Dodoma.*

Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi alikagua maendeleo ya ujenzi wa jengo la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali linaloendelea kujengwa kwenye mji wa Serikali, Mtumba jijini Dodoma.

Ujenzi wa jengo hilo unagharamiwa na Serikali kwa jumla ya shilingi bilioni 26. Hadi sasa ujenzi umefikia kiwango cha asilimia 73 na umegharimu jumla ya shilingi bilioni 16.

Dkt. Possi alimtaka mkandarasi, SUMA JKT na mshauri elekezi, TBA kuhakikisha kuwa jengo hilo linakamilika kwa kuzingatia viwango na ubora unaotakiwa ili liweze kutumika kwa muda mrefu. Pia, alimwelekeza mkandarasi kuwa kisima cha maji ya ardhini kilichochimbwa kitunzwe ili maji yake yaweze kutumika wakati wa msimu wa kiangazi na matumizi mbali mbali ikiwemo utunzaji wa mazingira ili kuifanya Dodoma kuwa ya kijani.

*"Nategemea kupata jengo lenye ubora na viwango vinavyotakiwa ili liweze kutumika kwa muda mrefu kwa lengo la kusogeza huduma karibu na wananchi na kuongeza tija na ufanisi katika mnyororo wa utoaji haki nchini,"* alisisitiza Dkt. Possi.

Pia, aliekeza kuwa jengo liishe mapema mwaka huu ili Ofisi ihamie Dodoma kwa kuwa Ofisi hii inafanya kazi kwa karibu na Mahakama ya Tanzania ambayo tayari imehamia Dodoma.

Dkt. Possi aliambatana na Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Kanali Saul Chiwanga, Meneja Ujenzi Kanda ya Mashariki wa SUMA JKT na ndugu Daniel Nkruma, Kaimu Meneja Miradi wa TBA.



*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi (aliyesimama katikati mbele) akiwa kwenye picha ya pamoja na wajumbe wa Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Mkandarasi - Suma JKT na mshauri elekezi, TBA baada ya ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa jengo la Ofisi hiyo unaoendelea katika Mji wa Serikali, Mtumba - Dodoma.*



*Muonekano wa jengo la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali linaloendelea kujengwa katika Mji wa Serikali, Mtumba - Dodoma.*



*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi (wa kwanza kushoto) akipatiwa maelezo na mkandarasi, Meneja Ujenzi Kanda ya Mashariki wa SUMA JKT, Kanali Saul Chiwanga kuhusu maendeleo ya ujenzi wa jengo la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakati wa ziara ya kukagua jengo hilo lililopo Mji wa Serikali, Mtumba - Dodoma.*

*Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Asha Hayeshi akitoa maelezo mafupi kuhusu maendeleo ya ujenzi wa jengo la Ofisi hiyo kwa Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi (hayupo pichani) alipotembelea mradi huo katika Mji wa Serikali, Mtumba - Dodoma.*



# Mpango Mkakati wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kufikia Dira 2050

***“OWMS inakuwa si tu kiranja katika kuendesha mashauri ya Serikali na taasisi zake bali pia ni kinara wa kuhakikisha kwamba Dira 2050 inafikiwa kwa kulinda rasilimali na maslahi mapana ya taifa.”***

Katika enzi ya mageuzi ya kitaifa, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 ya Tanzania tuitakayo inaweka malengo ya muda mrefu ya kuifanya Tanzania iwe taifa lenye uchumi imara, jamii yenye ustawi na huduma bora za kijamii kwa wote.

Dira hiyo inalenga kuleta maendeleo endelevu, ukuaji wa uchumi, uboreshaji wa miundombinu, sheria na utawala bora. Pia, kila taasisi ya umma inahitajika kuweka mikakati madhubuti ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kwa ustawi wa taifa.

Katika muktadha huo, OWMS ina jukumu la msingi la kisheria la kuishauri Serikali katika uendeshaji na usimamizi wa mashauri ya madai, usuluhishi, katiba, haki za binadamu na uchaguzi. Vile vile inatoa ushauri wa kisheria na maoni kuhusu sheria zinazohitaji maboresho.

Jukumu hili ni nyenzo muhimu ya kuhakikisha utekelezaji wa sera za Serikali unafuata utaratibu wa sheria na unajengeka kwa msingi thabiti wa kisheria.

Moja ya changamoto kuu za utekelezaji wa nyenzo za maendeleo ni ukosefu wa muundo wa kisheria unaoendana na malengo ya Dira 2050. Ili Serikali iweze kutekeleza miradi mikubwa ya maendeleo ikiwa ni pamoja na uwekezaji, uanzishaji wa taasisi mpya, mikataba ya ushirikiano wa sekta ya umma na binafsi na uboreshaji wa huduma za umma inahitaji sheria ambazo zinaboresha mazingira ya uwekezaji, usimamizi wa rasilimali na kulinda maslahi ya taifa.

Ili kuhakikisha Mpango Mkakati wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali unaleta tija katika kufikia malengo ya Dira 2050 ni muhimu kutunga na kufanya maboresho ya sheria zilizopo ili ziendane na malengo ya uchumi wa kisasa, uwekezaji, teknolojia na utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

Hatua hizi zitasaidia kuunda muundo thabiti wa kisheria ambao unaifanya Serikali kuondokana na utegemezi zaidi na kuweza kutekeleza miradi mikubwa bila vizuizi na kupunguza utata wa kisheria wakati wa utekelezaji wa miradi.

Moja ya sura ya mkakati wa OWMS ni kuendeleza uwezo wa Mawakili wa Serikali kwa kupata elimu ya kisasa na ujuzi wa kufanya kazi katika mazingira ya mabadiliko ya uchumi mathalani kuwapa mafunzo ya kitaaluma kuhusu ushirikiano wa sekta ya umma na binafsi na taratibu za uendeshaji wa mashauri kimataifa. Mafunzo hayo yanaongeza uwezo wao katika kuendesha mashauri ya madai na usuluhishi yanayotokana na miradi mikubwa ya maendeleo na mikataba ya kimataifa hatua itakayosaidia kufika malengo katika kutekeleza Dira 2050.

Mojawapo ya nguzo za Dira 2050 ni utawala bora, uwazi na uwajibikaji. OWMS inachangia moja kwa moja kuimarisha taswira ya Serikali kwa umma kwa kuendesha mashauri kwa ufanisi ili kuimarisha utendaji wa Serikali katika kuwaletea wananchi maendeleo.

Kwa kufanya haya, OWMS inakuwa si tu kiranja katika kuendesha mashauri ya Serikali na taasisi zake bali pia ni kinara wa kuhakikisha kwamba Dira 2050 inafikiwa kwa kulinda rasilimali na maslahi mapana ya taifa.




# Dkt. Possi: Viongozi ni Taswira ya Taasisi na Serikali kwa Jamii

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali iliendesha kikao cha faragha na mafunzo kwa wajumbe wa menejimenti ya Ofisi hiyo, ambayo yalifanyika jijini Dodoma. Vile vile viongozi hao walipata fursa ya kufanya tathmini ya utendaji kazi wao wa kila siku pamoja na mafunzo ya uongozi yanayohusu usimamizi na mgawanyo wa majukumu, usimamizi wa muda, itifaki na ustaarabu.

Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi alifungua mafunzo hayo na kuwaeleza wajumbe wa menejimenti ya Ofisi hiyo kuwa viongozi ni taswira ya taasisi na Serikali kwa ujumla. Pia, aliongeza kuwa kiongozi yeyote awe Mkuu wa Idara au Mkuu wa Kitengo atambue kuwa anabeba taswira ya taasisi anayofanyia kazi na Serikali kwa ujumla popote alipo, iwe kazi au unapoishi. Hivyo, ni muhimu kuzingatia sheria, taratibu, kanuni, maadili, mila na desturi za uongozi.

*“Kila mmoja ajitambue wadhifa alionao na bendera anayoipeperusha ni kwa niaba ya Serikali na kwa wale anaowaongoza. Tuwe walezi kwa kuzingatia kuwa muda mwingi tupo mahali pa kazi kuliko familia zetu,”* alisisitiza Dkt. Possi.

Aidha, aliongeza kuwa watu tunaofanya nao kazi wafurahie kufanya kazi na wewe badala ya kukasirika, tujitathmini na kutafakari utendaji kazi wetu ili kuwa na matokeo mazuri mahali pa kazi na kujipa muda wa kujisahihisha. Pia, tufanye kazi kwa kuzingatia sheria, taratibu na kanuni, tuwe wabunifu na tufanye ufuatiliaji wa majukumu.

Naye Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice E. Mtulo alisema kuwa kikao hicho cha faragha na mafunzo hayo ni muhimu kwa wajumbe wa menejimenti wa Ofisi hiyo ili kupata muda wa kutathmini utendaji kazi. Vile vile, ana amini kuwa mafunzo hayo yataleta mabadiliko katika taasisi, kuwawezesha kuwafahamu na kuwasimamia vizuri wasaidizi wao, kumiliki kazi zao, kufanya maamuzi kwa wakati na kuzingatia muda katika utekelezaji wa majukumu.

Akitoa mada kuhusu uongozi na mgawanyo wa majukumu kwa wajumbe wa OWMS, Afisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Uongozi, ndugu Kadari Singo, aliwapongeza viongozi wa Ofisi hiyo kwa kuandaa na kushiriki mafunzo hayo. Pia, alitoa rai kwao kujenga utaratibu wa kuwajenga wasaidizi wao ili wanapoondoka kwenye nafasi zao wawe na watu wa kutekeleza majukumu yao.

Aidha, Mhadhiri wa Chuo cha Diplomasia, ndugu Godwin Gonde Amani, aliwafundisha wajumbe wa menejimenti hiyo mada kuhusu itifaki na ustaarabu ambayo ilijikita kwenye masuala ya muonekano wa mtu, mavazi, mawasiliano, tabia, mienendo, matumizi ya akili ya kuzaliwa, kuheshimu mamlaka na madaraka ya kiongozi, kutambua, kujali na kuthamini uwepo wa kiongozi.

*“Iitifaki ni jambo muhimu Serikalini na katika uongozi kwa kuwa ni suala nyeti lina athari chanya na hasi baina yako binafsi na mtu mwingine katika muonekano wa mavazi, salamu, mazungumzo na mawasiliano,”* alisisitiza Mhadhiri Amani.

OWMS imekuwa na utaratibu wa kuendesha mafunzo kwa viongozi wa Ofisi hiyo na kufanya vikao vya faragha kwa ajili ya kutathmini utendaji kazi na utekelezaji wa majukumu mara moja kwa mwaka.

***“Iitifaki ni jambo muhimu Serikalini na katika uongozi kwa kuwa ni suala nyeti lina athari chanya na hasi baina yako binafsi na mtu mwingine katika muonekano wa mavazi, salamu, mazungumzo na mawasiliano.”***




*Bi. Alice E. Mtulo, Naibu Wakili Mkuu wa Serikali akizungumza na Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakati wa kikao cha faragha kilichofanyika jijini Dodoma.*




*Ndugu Kadari Singo, Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Uongozi akitoa mada kuhusu Ugawaji wa Majukumu na Usimamizi wa Muda kwa wajumbe wa Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakati wa kikao cha faragha kilichofanyika jijini Dodoma.*



*Ndugu Camilius Ruhinda, Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Mashauri na Udhibiti Ubora wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali akizungumza wakati wa kikao cha faragha kwa wajumbe wa menejimenti ya Ofisi hiyo kilichofanyika jijini Dodoma.*



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Prisca Ulomi akichangia mada kuhusu Ugawaji wa Majukumu na Usimamizi wa Muda wakati wa kikao cha faragha kwa viongozi wa Ofisi hiyo kilichofanyika jijini Dodoma.*



*Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Madai ya Ndani wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, ndugu Deodatus Nyoni akichangia mada kuhusu Ugawaji wa Majukumu na Usimamizi wa Muda wakati wa kikao cha faragha kwa viongozi wa Ofisi hiyo kilichofanyika jijini Dodoma.*

# Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi Ampongeza Mwanasheria Mkuu wa Serikali



*Mhe. Hamza Said Johari akiapa mbele ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan (hayupo pichani) kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwenye hafla fupi iliyofanyika Ikulu Chamwino Jijini Dodoma.*

Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi alimpongeza Mhe. Hamza Said Johari kwa kuteuliwa na kuapishwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Dkt. Possi alisema kuwa uteuzi huu umetokana na umahiri wake katika kutoa ushauri wa kisheria kwa Serikali, kufanya kazi bila kuchoka na kuwa tayari kusimamia masuala ya kisheria kwa kuzingatia Katiba, usawa na haki ili kuimarisha misingi ya utawala wa sheria na utawala bora kwa lengo la kuendelea kuwaletea wananchi maendeleo.

Aidha, Dkt. Possi alimtakia kheri na mafanikio Mhe. Johari katika utekelezaji wa majukumu yake. Pia, alitoa rai kwake ya kuendeleza ushirikiano uliopo kati ya Wizara ya Katiba na Sheria,

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Ofisi zote zilizopo kwenye mnyororo wa utoaji haki nchini. Hii itasaidia kutekeleza kwa vitendo dhana ya utoaji haki nchini kuendana na Dira 2050.

Akizungumza mara baada ya kuwasili katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Johari alimshukuru Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kumteua tena kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kuendelea kuishauri Serikali katika masuala yote ya kisheria.

*"Nimshukuru Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa imani yake kubwa kwangu na kuniteua tena kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kuendelea kuishauri Serikali kwa mujibu wa Katiba na Sheria, Namshukuru sana Mhe. Rais,"* alisema Mhe. Johari.

Mhe. Johari alitumia fursa hiyo kuwashukuru watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wadau wote waliopo kwenye mnyororo wa utoaji haki na kuwataka waendelee kufanya kazi kwa bidii na kutoa ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu yao.

Akitoa salamu za pongezi, Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria ndugu Eliakimu Maswi, alimpongeza Mhe. Johari kwa kuteuliwa na kuapishwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kuahidi kumpa ushirikiano wakati wote kwa lengo la kuongeza kasi ya utekelezaji wa majukumu ya ofisi hiyo.



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akimuapisha Mhe. Hamza Said Johari kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwenye hafla fupi iliyofanyika Ikulu Chamwino Jijini Dodoma.*

# OWMS Yawasilisha Taarifa ya Utekelezaji kwa Kamati ya Bunge



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice E. Mtulo akiwasilisha taarifa ya majukumu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali mbele ya kikao cha Kamati ya Kudumu  ya  Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria katika ukumbi wa Bunge jijini, Dodoma.*

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali iliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa majukumu yake mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kwenye ukumbi wa Bunge jijini Dodoma wakati wa kikao, kwa lengo la kutathmini utendaji kazi, changamoto na mafanikio ya Ofisi hiyo katika kusimamia na kuendesha mashauri ya Serikali.

Akizungumza na wajumbe wa kamati hiyo na viongozi wa OWMS, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro, alisema kuwa ushirikiano kati ya Kamati ya Bunge, Wizara ya Katiba na Sheria na OWMS ni jukwaa muhimu katika kuhakikisha maslahi ya nchi yanalindwa kupitia mifumo imara ya kisheria iliyopo nchini.

Dkt. Ndumbaro aliipongeza OWMS kwa kazi nzuri inayofanya na kueleza kuwa imeimarisha utendaji kazi Serikalini kutokana na uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi kwa weledi na ufanisi. Hatua hiyo imesaidia kuokoa fedha nyingi ambazo zitawezesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo nchini.

Mhe. Dkt. Ndumbaro alieleza kuwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ni daraja la kuhakikisha OWMS inapata rasilimali zote zinazohitajika ili kuendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Kwa upande wake, Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice E. Mtulo akiwasilisha mwelekeo wa OWMS kwa Mwaka wa Fedha 2026/27, alibainisha kuwa Ofisi itaendelea kujipanga vyema katika uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi ili kuhakikisha kila shauri linalofunguliwa na Serikali au dhidi ya Serikali linaendeshwa kwa kiwango cha juu na weledi.

Bi. Mtulo alieleza kuwa OWMS itahakikisha inafanyia kazi maelekezo na ushauri unaotolewa na Kamati huku akiahidi kuendelea kufanya kazi kwa karibu na Kamati, Wizara na taasisi zake kwa lengo la kuongeza chachu ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi katika kufikia malengo iliyojiwekea.

*"Tunatambua kuwa ushauri na maelekezo yanayotolewa na Kamati hii ni chachu ya mabadiliko ndani ya Ofisi yetu, tunaahidi kuendelea kufanya kazi kwa karibu na Kamati pamoja na Wizara ili kuhakikisha majukumu yetu yanatekelezwa kwa wakati na kwa ubora unaostahili,"* alisema Bi. Mtulo.

Kuelekea Dira 2050, Bi. Mtulo alieleza kuwa OWMS itaendelea na usimamizi madhubuti na uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi ili kuhakikisha rasilimali za nchi zinalindwa, jambo ambalo litasaidia kuvutia wawekezaji wa sekta mbalimbali na uboreshaji wa miundombinu ili kuchochea ukuaji wa uchumi na ustawi wa jamii.

Bi. Mtulo aliongeza kuwa OWMS itaendelea kuimarisha mifumo ya ndani ya TEHAMA na kuendelea kutoa mafunzo kwa watumishi wa kada zote ili kuhakikisha OWMS inaendana na kasi ya mabadiliko ya sayansi na teknolojia duniani ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu

***"Tunatambua kuwa ushauri na maelekezo yanayotolewa na Kamati hii ni chachu ya mabadiliko ndani ya Ofisi yetu, tunaahidi kuendelea kufanya kazi kwa karibu na Kamati pamoja na Wizara ili kuhakikisha majukumu yetu yanatekelezwa kwa wakati na kwa ubora unaostahili."***



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice E. Mtulo akiwasilisha taarifa ya majukumu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali mbele ya kikao cha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria katika ukumbi wa Bunge jijini, Dodoma.*



*Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro (Mb), akifurahia jambo wakati viongozi wa Wizara ya Katiba na Sheria na taasisi zilizo chini yake wakiwasilisha taarifa ya majukumu ya taasisi zao katika ukumbi wa Bunge jijini, Dodoma.*

# Kliniki za Sheria Kutatua Kero za Wananchi Zenye Mfumo wa Sheria



*Mhe. Albert Chalamila, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam akizungumza na wananchi wakati akizindua Kamati za Ushauri wa Kisheria Ngazi ya Mkoa na Wilaya na Kliniki ya Sheria Bila Malipo kwenye viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam.*

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilishiriki kwenye uzinduzi wa Kamati za Ushauri wa Sheria ngazi ya Mkoa na Wilaya na Kliniki ya Sheria Bila Malipo uliofanyika kwenye viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam.

Mhe. Albert Chalamila, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Saalaam alizindua Kamati za Ushauri wa Sheria ngazi ya Mkoa na Wilaya na Kliniki ya Sheria Bila Malipo ambapo alisema kliniki hizo zinatarajiwa kutatua kero za kisheria za wananchi na kupunguza malalamiko.

*"Kliniki hizi za kisheria zitatusaidia viongozi kushughulikia miradi ya maendeleo ya wananchi badala ya kushughulikia migogoro ya kisheria ya wananchi,"* alisisitiza Mhe. Chalamila.

Pia, aliongeza kuwa kamati za kisheria zitapunguza migogoro baina ya wananchi na Serikali na kuwasaidia viongozi kutoa maamuzi yaliyo katika mfumo wa kisheria na zitawawezesha Mawakili kusimamia utawala wa sheria.

Vile vile, alimpongeza na kumshukuru Dkt. Ally Possi, Wakili Mkuu wa Serikali kwa kushiriki uzinduzi huo ili Mawakili wa Serikali waweze kutatua kero za wananchi kwa kuwa wananchi wengi wanalumbana sana katika misingi ya kisheria kwa sababu hawafahamu sheria katika jamii yetu.

Akizungumza wakati anahudumia wananchi, Mhe. Hamza Johari, Mwanasheria Mkuu wa Serikali alisema lengo la Ofisi yake ni kusogeza huduma za kisheria kwa wananchi ili kupunguza migogoro na kuipunguzia mahakama mlundikano wa kesi.

Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ndugu Samwel Maneno, aliwapongeza wananchi kwa kujitokeza kwa wingi kushiriki uzinduzi huo. Pia, aliwajulisha kuwa Ofisi yake iko tayari kutoa elimu ya kisheria kwao na kuwaongoza kupata haki zao pale zinapovunjwa au kuelekea kuvunjwa ili kuleta utulivu katika jamii na utawala wa sheria.

Kliniki ya sheria iliyozinduliwa ilitoa msaada wa kisheria kwa wananchi kwa muda wa wiki moja baada ya uzinduzi. Mawakili wa Serikali na Mawakili kutoka Chama cha Mawakili wa Tanganyika (TLS) waliendesha Kliniki hiyo.




*Mhe. Albert Chalamila, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, akiwa kwenye picha ya pamoja na Viongozi na Mawakili wa Serikali baada ya uzinduzi wa Kamati za Ushauri wa Kisheria Ngazi ya Mkoa na Wilaya na Kliniki ya Sheria Bila Malipo uliofanyika kwenye viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam.*




*Dkt. Ally Possi, Wakili Mkuu wa Serikali (aliyeketi kulia) akizungumza na Mkurugenzi wa Taifa wa Mashtaka, ndugu Slyvester Mwakitalu kabla ya uzinduzi wa Kamati za Ushauri wa Kisheria ngazi ya Mkoa na Wilaya na Kliniki ya Sheria Bila Malipo uliofanyika kwenye viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam.*




*Mhe. Hamza Johari, Mwanasheria Mkuu wa Serikali (aliyeketi katikati), akitoa msaada wa sheria kwa mwananchi wakati wa Kliniki ya Sheria Bila Malipo uliofanyika kwenye viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam.*



*Baadhi ya Mawakili wa Serikali wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakimsikiliza Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Mhe. Albert Chalamila (hayupo pichani) wakati akizindua Kamati za Ushauri wa Kisheria Ngazi ya Mkoa na Wilaya na Kliniki ya Sheria Bila Malipo kwenye viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam.*

# Wakili Mfawidhi Mkoani Manyara Azitaka Mamlaka Kujiepusha na Utoaji wa Hati kwa Mwananchi Zaidi ya Mmoja.

Mamlaka mkoani Manyara zimeshauriwa kuepuka kutoa hati ya umiliki wa ardhi kwa mwananchi zaidi ya mmoja ili kuepuka migogoro isiyo ya lazima katika jamii hatua ambayo itasaidia kuwaletea wananchi maendeleo.

Ushauri huo ulitolewa na ndugu Lameck Butuntu, Wakili Mfawidhi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ushauri wa Kisheria ya Mkoa wa Manyara wakati wa Kliniki ya kutoa elimu ya msaada wa kisheria iliyofanyika wilaya ya Hanang' mkoani Manyara.

Akieleza faida za kuepuka kumpa hatimiliki ya ardhi mtu zaidi ya mmoja, Wakili Mfawidhi Butuntu alisema kuwa itasaidia kupunguza migogoro kati ya wananchi na Serikali kwa kiasi kikubwa na kufanya jamii kubaki na amani na utulivu na kuendelea na shughuli za kujiletea maendeleo.

Aliongeza kuwa mwananchi akiwa na uhakika wa kumiliki ardhi bila mgogoro, hujiamini na kuwekeza kwenye miradi ikiwemo Sekta ya Ujenzi, Bashara na Kilimo. Vile vile, atakuwa na vigezo vya kupata mikopo nafuu kutoka kwenye benki na taasisi za fedha kwa lengo la kuongeza uwekezaji. Hatua hii itasaidia kuzalisha ajira nyingi kwa vijana na kutatua tatizo la ajira nchini.

Alifafanua kuwa kuepuka kutoa hati ya matumizi ya ardhi kwa mwananchi zaidi ya mmoja kutasaidia kuvutia wawekezaji nchini. Hatua hii itasaidia kuboresha mazingira mazuri ya uwekezaji nchini ambapo fedha zitakazopatikana zitawezesha kutekeleza miradi mbalimbali kwa lengo la kuwaletea wananchi maendeleo.

Aidha, kiongozi huyo alitoa rai kwa taasisi za Kuzuia na Kupambana na Rushwa mkoani humo kufanya uchunguzi wa kina ili kubaini watumishi wa Wizara, taasisi na Idara za Serikali wanaoshiriki kutoa hatimiliki kwa mwananchi zaidi ya mmoja ili waweze kuchukuliwa hatua za kisheria.

Wakati wa kliniki hiyo ya kutoa elimu na msaada wa kisheria, Mawakili wa Serikali walifanikiwa kufanya usuluhishi wa mgogoro wa madai kati ya mwananchi na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ambaye pikipiki yake ilipotea kwenye Ofisi za TRA baada ya pikipiki yake kushikiliwa kwa miaka minne. Katika mgogoro huo mwananchi huyo alidai fidia ya shilingi milioni 45, ambapo baada ya usuluhishi Mamlaka ya Mapato Tanzania ilikubali kumlipa mwananchi huyo pikipiki mpya yenye thamani ya shilingi milioni 3.6.

Akizungumzia kuhusu Kliniki hiyo, Mkurugenzi wa Uratibu

na Huduma za Ushauri wa Kisheria Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Bi. Neema Ringo alisema wananchi walijitokeza kwa wingi kupata huduma za ushauri wa kisheria katika Kliniki hiyo ambapo wengi wao walikuwa na migogoro ya ardhi, ndoa, ajira na mirathi.

Aidha, Bi. Neema Ringo alisema Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilifanikiwa kutatua baadhi ya migogoro hapohapo wakati wa Kliniki na baadhi ya changamoto za kisheria zilichukuliwa kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria.

Kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Manyara, Bi. Cecilia Sulle aliishukuru Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kushirikiana na Mkuu wa Mkoa kwa kuleta huduma ya Kliniki ya Sheria bila Malipo.

*"Nashukuru sana Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mkuu wa Mkoa kwa huduma hii, sisi wajane na watu wa hali ya chini tumekuwa tukikosa haki zetu, lakini kwa kliniki hii nimeweza kupata msaada na kupata haki yangu,"* alisema Bi. Cecilia.

Kliniki ya elimu na msaada wa kisheria bila Malipo iliratibiwa na kuendeshwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuanzia tarehe 19 Januari, 2026 na kukamilika tarehe 25 Januari, 2026 mkoani Manyara wilaya ya Hanang' katika viwanja vya Mount Hanang Katesh.




*Baadhi ya Wananchi wa Mkoa wa Manyara wakipata msaada wa kisheria bila malipo wakati wa uzinduzi wa Kamati za Ushauri wa Kisheria ngazi ya Mkoa na Wilaya na Kliniki ya Sheria Bila Malipo.*



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice E. Mtulo akizungumza na wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakati akifungua Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi hiyo uliofanyika Kibaha mkoani Pwani.*

# Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice E. Mtulo Awahimiza Watumishi wa OWMS Kufanya Kazi kwa Bidii

Watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wamehimizwa kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa bidii, weledi na ufanisi kwa kutimiza wajibu wao ili kusaidia Ofisi hiyo kufikia malengo iliyojiwekea kwa wakati.

Wito huo ulitolewa na Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice E. Mtulo wakati akifungua Mkutano wa Kwanza wa Kikao cha Pili cha Baraza la Wafanyakazi kilichofanyika tarehe 3 na 4 Disemba 2025, Kibaha mkoani Pwani.

Bi. Mtulo alisisitiza kuwa ni muhimu kwa watumishi wa OWMS kuendelea kufanya kazi kwa umakini na kuhakikisha wanatumia vizuri muda wakati wowote wanapokuwa mahala pa kazi. Vile vile, kufanya kazi kwa kufuata sheria, taratibu na kanuni za utumishi wa umma.

Alieleza kuwa Baraza hili ni fursa ya kubadilishana mawazo, kutathmini utendaji kazi na kutengeneza mikakati ya kuboresha utoaji wa huduma za kisheria ili kusaidia Serikali kushinda mashauri yanayofunguliwa ndani na nje ya nchi.

Aliongeza kuwa Baraza hili limekuwa ni jukwaa muhimu kwa OWMS kutathmini utendaji

kazi na kupanga mikakati itakayosaidia OWMS kufikia malengo yake ya kitaasisi ndani ya kipindi cha Mwaka wa Fedha 2025/26.

Bi. Mtulo alitumia mkutano huo kuwakumbusha watumishi wa Ofisi kuwa wana wajibu wa kuelewa malengo ya Ofisi kwa mwaka wa fedha husika. Vile vile, wanatakiwa kufanahamu bajeti iliyotengwa lazima itumike kwa tija na kwa kuzingatia vipaumbele vilivyowekwa ili kufikia malengo ya kimkakati ya taasisi.

Aidha, Bi. Mtulo aliwataka Wakuu wa Idara, Sehemu na Vitengo kuendelea kusimamia utekelezaji wa malengo ya muda mrefu na mfupi ili kuhakikisha mashauri yanaendeshwa kwa ufanisi.

Akizungumzia matumizi ya TEHAMA, Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Mtulo alisisitiza umuhimu wa watumishi wa OWMS kutumia mifumo ya TEHAMA ili kuendana na kasi ya mabadiliko ya sayansi na teknolojia ulimwenguni.

Alifafanua kuwa matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika kusimamia mashauri ya Serikali ni muhimu kwa kuwa yanasaidia kurahisisha ufuatiliaji wa mashauri na kuongeza uwazi katika utendaji kazi wa kila siku. Hatua hii itasaidia kuokoa muda, kupunguza mrundikano wa mashauri na hivyo haki kutolewa kwa wakati.

Aliahidi kuwa Ofisi itaendelea kuboresha mazingira ya kazi ili kuwapa watumishi ari ya kutoa huduma bora hususan katika kutekeleza jukumu lake la kuendesha mashauri ya Madai, Usuluhishi, Katiba, Haki za Binadamu na Uchaguzi.

Wakati wa mkutano huo, wajumbe wa Baraza walipata fursa ya kuchagua viongozi wapya ambapo Bi. Susana Joseph alichaguliwa kuwa Katibu na Ndugu Athumani Zunda alichaguliwa kuwa Katibu Msaidizi.



*Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Asha Hayeshi akimkaribisha Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Bi. Alice E. Mtulo (hayupo pichani) kufungua Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali uliofanyika Kibaha mkoani Pwani.*



*Bi. Sabina Yongo, Mjumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali akichangia mada kuhusu taarifa ya rasimu ya uanzishwaji wa SACCOS ya Ofisi hiyo wakati wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi uliofanyika Kibaha mkoani Pwani.*





*Baadhi ya Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakimsikiliza Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice E. Mtulo (hayupo pichani) wakati akifungua mkutano wa Baraza hilo uliofanyika Kibaha mkoani Pwani.*




*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice E. Mtulo (aliyesimama katikati) akiwaongoza wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kuimba wimbo wa mshikamano daima wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa Baraza hilo uliofanyika Kibaha mkoani Pwani.*






*Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Mhe. Albert Chalamila akizungumza na wanawake wa Mkoa wa Dar es Salaam wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wanawake Duniani yaliyofanyika kwenye viwanja vya Barafu Mburahati Jijini Dar es Salaam.*

# Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Yashiriki Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani

Wanawake wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wameungana na wanawake wengine duniani kusherehekea maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wanawake Duniani yaliyofanyika tarehe 8 Machi, 2026 kwenye Viwanja vya Barafu Mburahati, Jijini Dar es Salaam.

Maadhimisho hayo mkoani Dar es Salaam yaliongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Mhe. Albert Chalamila ambapo yaliwakutanisha wanawake kutoka Wizara na taasisi mbalimbali za Serikali na binafsi. Maadhimisho hayo yalilenga kuwakumbusha wanawake mchango wao katika maendeleo ya jamii na uchumi kwa mustakabali wa taifa.

Akizungumza wakati wa maadhimisho, Mhe. Chalamila aliitaka jamii kuadhimisha siku hiyo kwa vitendo badala ya maneno pekee. Vile vile, alihimiza jamii kuwasaidia wanawake na watoto wenye mahitaji maalumu ili

kuwawezesha na kuwainua kiuchumi.

Naye Mhe. Albert Msando, Mkuu wa Wilaya ya Ubungo aliwahimiza wanawake wa mkoa wa Dar es Salaam kutumia fursa mbalimbali za uwezeshaji zinazotolewa na wilaya ili kujikwamua kiuchumi na kuepuka unyanyasaji wa kijinsia unaosababishwa na utegemezi.

Bi. Devota Ngulugulu, Mhasibu Mkuu wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali alisema kuwa ushiriki wa Ofisi unalenga kuwahimiza wanawake kutumia fursa za kiuchumi na rasilimali zilizopo nchini ili kujikwamua na kuimarisha kipato chao.

Alibainisha kuwa Ofisi inatekeleza kauli mbiu ya mwaka huu kwa vitendo kwa kuhakikisha watumishi wanawake ndani ya OWMS wanapata haki sawa katika nafasi za uongozi na mafunzo. Hatua itakayowasaidia kuwajengea uwezo kwenye kada zao na kuwa viongozi bora watakaosaidia kuliletea taifa maendeleo.

Akizungumzia kuhusu umuhimu wa siku hii, Bi. Ngulugulu alieleza siku hiyo ni ya muhimu kwa kila mwanamke wa OWMS kwa kuwa inatoa fursa ya kuimarisha mshikamano miongoni mwa watumishi wanawake na kuthamini mchango wao mkubwa katika kutekeleza majukumu ya OWMS.

Maadhimisho ya mwaka huu yaliongozwa na kauli mbiu isemayo, ***“Haki kwa wanawake na wasichana ni msingi wa maendeleo jumuishi kufikia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.’’*** Dhumuni la kauli mbiu hiyo ni kuhamasisha jamii kutambua umuhimu wa kuhakikisha wanawake na wasichana wanapata haki na fursa sawa katika elimu, uchumi na uongozi. Hatua hiyo itachangia kufanikisha maendeleo endelevu ya taifa.





*Baadhi ya wanawake wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakielekea kushiriki Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wanawake Duniani viwanja vya Barafu Mburahati Jijini Dar es Salaam .*




*Bi. Alice E. Mtulo, Naibu Wakili Mkuu wa Serikali akizungumza na Wanawake wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakati akifungua mafunzo kuhusu afya ya akili yaliyofanyika Jijini Dar es Salaam.*



*Bi. Alice E. Mtulo, Naibu Wakili Mkuu wa Serikali (aliyeketi katikati) akiwa kwenye picha ya pamoja na watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kuelekea Siku ya Wanawake Duniani kwenye hafla iliyofanyika Jijini Dar es Salaam.*




*Bi. Alice E. Mtulo, Naibu Wakili Mkuu wa Serikali (aliyesimama kulia) akimkabidhi hundi Malkia wa Nguvu wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Bi. Stella Machoke kuelekea Siku ya Wanawake Duniani kwenye hafla iliyofanyika Jijini Dar es Salaam.*




*Bi. Prisca Ulomi, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali akimkabidhi Bi. Alice E. Mtulo, Naibu Wakili Mkuu wa Serikali (wa pili kulia) zawadi ya picha yake ya kuchorwa kuelekea Siku ya Wanawake Duniani iliyofanyika Jijini Dar es Salaam.*




*Bi. Mwajuma Sihiyana, Katibu Sheria wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali akimkabidhi Bi. Alice E. Mtulo, Naibu Wakili Mkuu wa Serikali (wa pili kulia) zawadi ya picha yake ya kuchorwa kwa niaba ya wanawake wa Ofisi hiyo kuelekea Siku ya Wanawake Duniani iliyofanyika Jijini Dar es Salaam.*

# Habari Picha



*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi akifafanua jambo baada ya uwasilishaji wa randama ya mpango na bajeti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2026/27 uliofanywa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, ndugu Eliakim Maswi mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria tarehe 28 Machi, 2026 kwenye ukumbi wa Bunge jijini Dodoma*



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo (wa pili kulia) akifuatilia uwasilishaji wa randama ya mpango na bajeti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2026/27 uliofanywa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, ndugu Eliakim Maswi (hayupo pichani) mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria tarehe 28 Machi, 2026 kwenye ukumbi wa Bunge jijini Dodoma*



*Bi. Alice E. Mtulo, Naibu Wakili Mkuu wa Serikali akizungumza na waajiriwa wapya wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakati akifunga mafunzo elekezi yaliyofanyika Kibaha mkoani Pwani.*

# Waajiriwa Wapya Wapewa Mafunzo ya Sheria, Taratibu na Kanuni za Utumishi wa Umma

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali iliendesha mafunzo kwa waajiriwa wapya wa Ofisi hiyo kuhusu sheria, taratibu na kanuni za utumishi wa umma ili waweze kufahamu utendaji kazi wa Serikali na kuwawezesha kutekeleza majukumu ya Ofisi kwa niaba ya Serikali.

“Mafunzo mliyopatiwa kuhusu sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma naamini yatawawezesha kufahamu utendaji kazi wa Serikali hivyo mtakuwa kwenye nafasi nzuri ya kutekeleza majukumu ya OWMS kwa kuzingatia taaluma ya kila mmoja wenu katika eneo lake la kazi,” alisema Bi. Mtulo.



*Bi. Alice E. Mtulo, Naibu Wakili Mkuu wa Serikali (aliyesimama katikati) akiwa kwenye picha ya pamoja na watumishi wapya (waliosimama nyuma) wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali baada ya kufunga mafunzo elekezi kwa watumishi hao yaliyofanyika Kibaha mkoani Pwani.*

Pia, ameongeza kuwa OWMS inajishughulisha na uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi kwa niaba ya Serikali hivyo waajiriwa wapya wanatakiwa kuhakikisha wanatekeleza majukumu ya msingi kwa wakati.

Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu wa OWMS, Bi. Asha Hayeshi alisema waajiriwa wapya wa Ofisi wamepatiwa mafunzo kuhusu sheria, taratibu na kanuni za utumishi wa umma, maadili ya utumishi wa umma, utunzaji wa kumbukumbu na siri za Ofisi, mawasiliano na mahusiano mahali pa kazi, haki na wajibu wa mtumishi wa umma na majukumu ya Ofisi hiyo.

Bi. Alice E. Mtulo, Naibu Wakili Mkuu wa Serikali alifunga mafunzo hayo yaliyotolewa kwa waajiriwa wapya wa kada mbalimbali za Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali yaliyofanyika kwa siku tatu Kibaha mkoani Pwani.





*Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Asha Hayeshi akiwasilisha majukumu ya Idara hiyo kwa waajiriwa wapya wa Ofisi hiyo wakati wa mafunzo elekezi yaliyofanyika Kibaha mkoani Pwani.*



*Mkurugenzi Idara Usuluhishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, ndugu Saddy Sevingi akiwasilisha majukumu ya Idara hiyo kwa waajiriwa wapya wa Ofisi hiyo wakati wa mafunzo elekezi yaliyofanyika Kibaha mkoani Pwani.*



*Bi. Mercy Kyamba, Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Udhibiti Ubora wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali akiwasilisha majukumu ya Idara ya Usimamizi wa Mashauri na Udhibiti Ubora kwa waajiriwa wapya wa Ofisi hiyo wakati wa mafunzo elekezi yaliyofanyika Kibaha mkoani Pwani.*



*Ndugu Azizi Makaburi, Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali akiwasilisha majukumu ya Kitengo hicho kwa waajiriwa wapya wa Ofisi hiyo wakati wa mafunzo elekezi kwa watumishi hao yaliyofanyika Kibaha mkoani Pwani.*



*Baadhi ya waajiriwa wapya wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakimsikiliza Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice E. Mtulo (hayupo pichani) wakati akifunga mafunzo elekezi kwa watumishi hao yaliyofanyika Kibaha mkoani Pwani.*



*Mhe. Salma Maghimbi, Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Dar es Salaam akimkabidhi zawadi Wakili wa Serikali OWMS ndugu Mkama Msalama baada ya kuibuka mshindi wa kwanza wa mbio za mita mia wakati wa Bonanza la nusu mwaka lililoandaliwa na Mahakama ya Tanzania Jijini Dar es Salaam.*

# Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Yashiriki Bonanza la Mahakama

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, ilishiriki Bonanza la Michezo lililoandaliwa na Mahakama ya Tanzania Kanda ya Dar es Salaam kwa lengo la kuongeza ushirikiano na kuimarisha afya za watumishi wa taasisi zilizo kwenye mnyororo wa utoaji haki nchini.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa bonanza hilo, Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam, Mhe. Salma Maghimbi aliwahimiza watumishi hao kujenga tabia endelevu ya kufanya mazoezi ili kuepuka uwezekano wa kupata magonjwa yasiyoambukiza.

Alieleza kuwa uwepo wa bonanza unatokana na utekelezaji wa nguzo ya tatu ya Mpango Mkakati wa Mahakama ya Tanzania unaohimiza uimarishaji wa imani ya wananchi na ushirikishwaji wa wadau kwenye mnyororo wa utoaji haki nchini.

Kiongozi huyo aliendelea kuwakumbusha watumishi kuwa wana wajibu wa kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa bidii na weledi ikiwa ni pamoja na kuongeza ubunifu ili kuleta matokeo chanya na tija. Hatua hiyo itaongeza utoaji wa huduma ubora kwa kuzingatia sheria, taratibu na miongozo inayotolewa na viongozi wa Serikali katika kutekeleza

majukumu yao ya kila siku.

Mhe. Maghimbi alisisitiza kuwa kufanya mazoezi ni jambo muhimu katika kuimarisha afya na hivyo inasaidia kuongeza ufanishi katika utekelezaji wa majukumu mahali pa kazi.

Aliongeza kuwa afya njema inapatikana kwa kuwa na mtindo bora wa maisha unaozingatia ulaji unaofaa, kufanya mazoezi ya mwili na kuepuka matumizi ya sigara na tumbaku. Utaratibu huu utasaidia watumishi kukabiliana na magonjwa sugu yasiyoambukiza kama vile kisukari, saratani, shinikizo la damu na uzito uliopitiliza ili kulinda nguvu kazi za watumishi.

Mhe. Jaji Maghimbi aliwasisitiza watumishi kutenga muda wa kufanya mazoezi na kushiriki michezo mbalimbali hatua itakayosaidia kujenga umoja na ushirikiano miongoni mwa taasisi zilizopo kwenye mnyororo wa utoaji haki nchini.

Mwenyekiti na mratibu wa bonanza hilo, Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania Mhe. Anold Kerikiano alisema kuwa bonanza hili si kwa ajili ya kuimarisha afya za watumishi peke yake bali pia ni kuimarisha mahusiano kati ya Mahakama na wadau wake.

Akifafanua umuhimu wa watumishi kushiriki zoezi hilo, Mhe. Jaji Keriakano alieleza kuwa kupitia bonanza hilo watumishi wataweza kuimarisha afya, kushirikiana na kupendana hatua inayoweza kufanikisha utoaji huduma bora na kwa wakati.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Asha Hayeshi alisema kuwa ushiriki wa OWMS utasaidia kujenga ushirikiano miongoni mwa watumishi pamoja na kuendelea kujenga taswira ya Ofisi kwa wadau wetu.

Wakili wa Serikali wa OMWS ndugu Boaz Msofe aliwashukuru waratibu kwa kuandaa bonanza hilo. Vile vile, aliwaomba waratibu waendelee kuandaa bonanza kama hilo kwa kuwa pamoja na kuimarisha afya limekuwa daraja la kuongeza mahusiano miongoni mwa washiriki na wadau.



*Wachezaji wa Timu ya Kamba ya Wanawake wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakivuta kamba dhidi ya timu ya wanawake ya Wizara ya Viwanda na Biashara katika mchezo uliofanyika kwenye viwanja vya Furahisha jijini Mwanza.*




# Mahakama Yatupilia Mbali Shauri la Kupinga Tume ya Uchunguzi wa Matukio ya Uvunjifu wa Amani

Shauri la Mapitio Namba 32537 la 2025 la kupinga uundwaji wa Tume ya Uchunguzi wa Matukio ya Uvunjifu wa Amani yaliyotokea nchini wakati na baada ya Uchaguzi Mkuu wa tarehe 29 Oktoba 2025 lilifunguliwa Mahakama Kuu masjala ndogo ya Dar es salaam. Shauri hilo lilifunguliwa na Bi. Rosemary Mwakitwange na wenzake watatu dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na wajumbe wa Tume ya Uchunguzi.

Katika shauri hilo, waleta maombi waliiomba Mahakama Kuu, kupitia utaratibu wa mapitio ya Mahakama, itoe amri ya kufuta uamuzi wa Mheshimiwa Rais wa kuunda na kuteua wajumbe wa Tume hiyo tarehe 18 Novemba, 2025. Walidai kuwa Rais alivuka mipaka ya mamlaka yake ya kisheria wakati wa kuunda Tume hiyo.

Shauri hilo liliendeshwa na kusimamiwa na jopo la Mawakili wa Serikali kutoka Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa niaba ya Serikali.

Baada ya kusikiliza hoja za pande zote, tarehe 13 Machi 2026, Mahakama Kuu imetupilia mbali shauri hilo, ikieleza kuwa Mheshimiwa Rais alitumia mamlaka aliyonayo kisheria chini ya Kifungu cha 3 cha Sheria ya Tume za Uchunguzi, Sura ya 32, na kwamba hakuvunja mamlaka yake ya kisheria katika kuunda Tume hiyo.

Mahakama imeeleza kuwa kwa mujibu wa Kifungu cha 3 cha Sheria ya Tume za Uchunguzi, Sura 32 Rais ana mamlaka ya kuunda Tume na kuteua wajumbe wake.

Mahakama pia ilibainisha kuwa hakuna ushahidi uliowasilishwa mahakamani unaoonesha kuwa Rais alienda kinyume na matakwa ya sheria hiyo wakati wa kuunda Tume. Aidha, Mahakama haikuona uwepo wa upendeleo (bias) katika uteuzi wa wajumbe wa Tume, kwa kuwa sheria inampa Rais mamlaka ya kufanya uteuzi huo.

Kutokana na sababu hizo, Mahakama imehitimisha kuwa maombi ya walalamikaji hayakuwa na msingi wa kisheria, hivyo yakatupiliwa mbali.




*Bi. Mercy Kyamba, Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Udhibiti Ubora wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali akizungumzia ushirikiano uliopo kati ya Ofisi hiyo na Kituo cha Kimataifa cha Usuluhishi Tanzania wakati wa mkutano na waandishi wa habari kuhusu mafunzo na kongamano la ushirikishwaji wa wanawake kwenye utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala yaliyofanyika Jijini Dar es Salaam.*

# OWMS Yashiriki Kuandaa Mafunzo na Kongamano la Wanawake la Utatuzi wa Migogoro Kwa Njia Mbadala

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na Kituo cha Kimataifa cha Usuluhishi Tanzania (Tanzania International Arbitration Centre – TIAC) ilifanya maandalizi ya kuendesha mafunzo na kongamano la ushirikishwaji wa wanawake kwenye utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala. Lengo ni kuongeza idadi ya wanawake waliothibitishwa kwenye ngazi ya maamuzi na ushiriki kwenye utatuzi wa migogoro ndani na nje ya nchi.

Hayo yalielezwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa TIAC, ndugu Godson Nyange wakati akizungumza na waandishi wa habari kwenye ukumbi wa Wakili House, Dar es Salaam ili kuhabarisha umma kuhusu matukio hayo ambayo yalifanyika tarehe 24 hadi 27 Machi, 2026 jijini Dar es Salaam.

Kongamano hilo liliongozwa na kauli mbiu isemayo, ***"Kutoka Majadiliano hadi Hatua: Kuendeleza Ushirikishwaji wa Wanawake katika Utatuzi wa Migogoro kwa Njia Mbadala."*** Kongamano hilo

liliwaleta pamoja wataalamu wa sheria, watunga sera, wanataaluma, viongozi wa biashara, wataalamu wa utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala pamoja na wataalamu kutoka kada mbalimbali ili kuzitathimini kwa kina hatua za kuongeza ushiriki wa wanawake katika utatuzi wa migogoro.

Kongamano hilo lilitanguliwa na mafunzo yaliyoongozwa na mada isemayo, *"Kujenga Uwezo na Kujiamini kwa Wanawake katika Utatuzi Mbadala wa Migogoro."*

"Kihistoria, Sekta ya Utatuzi wa Migogoro kwa Njia Mbadala imekuwa ikitawaliwa zaidi na wanaume, huku wanawake wakiwa wachache katika nafasi za usuluhishi, upatanishi na majukumu mengine ya utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala hasa katika nafasi za juu za kufanya maamuzi," alifafanua ndugu Nyange.

Ndugu Nyange aliongeza kuwa, hali hii imeonekana duniani kote na barani Afrika ambapo tafiti zinaonyesha takribani asilimia 72 ya wasuluhishi katika kesi zinazohusiana na Afrika ni wanaume, wakati asilimia 28 tu ni wanawake. Vile vile, wanawake wanawakilisha takribani asilimia 29 hadi 34 ya uteuzi wa wasuluhishi katika taasisi kubwa za kimataifa za usuluhishi

Akizungumza kwa niaba ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Mercy Kyamba, Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Udhibiti Ubora alisema OWMS inashirikiana na TIAC kuendesha mafunzo na kufanya kongamano kwa kuwa OWMS pamoja na majukumu mengine, imekasimiwa na kupewa dhamana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kusimamia na kuendesha mashauri ya usuluhishi ndani na nje ya nchi kwa niaba ya Serikali.

Bi. Kyamba alisema uwepo wa mafunzo na kongamano ni dhamira ya pamoja ya TIAC na OWMS ya kuimarisha nafasi ya wanawake katika usuluhishi, upatanishi na mifumo mingine ya utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala. Mafunzo yaliendeshwa na wataalam wabobezi wa ndani na nje ya nchi na yalilenga kuwapatia wanawake maarifa, ujuzi wa vitendo na kujiamini kunakohitajika ili kushiriki kikamilifu katika michakato ya utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala.

Aidha, mafunzo yaliyotolewa yalihusu misingi ya usuluhishi na upatanishi; ujuzi wa vitendo katika majadiliano na usimamizi wa migogoro; viwango vya maadili na wajibu wa kitaaluma katika utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala; njia za kujenga taaluma na kupata ithibati katika utatuzi wa migogoro kwa njia




*Ndugu Godson Nyange, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Kituo cha Kimataifa cha Usuluhishi Tanzania (TIAC) akiongea na waandishi wa habari kuhusu mafunzo na kongamano la ushirikishwaji wa wanawake kwenye utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala yaliyofanyika Jijini Dar es Salaam.*

mbadala; na mikakati ya kujenga kujiamini na uwepo wa kitaaluma katika mashauri ya utatuzi wa migogoro.

Kongamano hilo lilikuwa ni jukwaa la kiwango cha juu la kujadili namna ya kuongeza ushiriki wa wanawake katika utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala. Majadiliano ya jopo la wataalamu yaliwakutanisha wadau mashuhuri katika kuchambua masuala muhimu kuhusu nafasi ya wanawake katika kuimarisha mifumo ya utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala; msaada wa taasisi katika kukuza wanawake katika usuluhishi na upatanishi; kujenga mitandao ya kitaaluma na fursa za ulezi kwa wataalamu wapya wa utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala; na athari pana ya utofauti wa kijinsia katika utoaji haki na imani ya kibiashara.

Mkurugenzi Mtendaji wa TIAC, Bi. Magreth Magoma alisema mafunzo na kongamano hilo ni sehemu ya juhudi pana za TIAC za kukuza matumizi na maendeleo ya utatuzi mbadala wa migogoro nchini Tanzania na katika ukanda mzima wa Afrika Mashariki. Hivyo, mafunzo hayo yamechangia kujenga mfumo madhubuti na unaoaminika wa utatuzi wa migogoro unaosaidia upatikanaji wa haki, uhakika wa biashara na kuimarisha uwekezaji.

Bi. Magoma aliongeza kuwa kupitia uwepo wa Sheria ya Usuluhishi nchini ya mwaka 2020 ambayo inaelekeza kuwa mtu yeyote anayetaka kufanya usuluhishi lazima apate ithibati kutoka Wizara ya Katiba na Sheria.

"Sheria hii ilianza utekelezaji wake mwaka 2021 ambapo hadi sasa Wizara imewapatia ithibati na kuwathibitisha jumla ya wanaume 444 katika eneo la usuluhishi na wanawake 89; majadiliano wanaume 162 na wanawake 38; wapatanishi wanaume 142 na wanawake 56; na upatanishi wanaume 77 na wanawake 14," alifafanua Bi. Magoma.

Mafunzo na kongamano hilo liliangazia umuhimu wa uwiano wa kijinsia katika utatuzi wa migogoro, kujadili mikakati ya kuongeza uelewa na ushiriki na uongozi wa wanawake katika utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala. Hii itawawezesha wanawake kuimarisha taaluma zao, kuchangia mfumo wa utatuzi wa migogoro ulio na uwiano, unaojumuisha wadau wote na unaoaminika zaidi.




*Bi. Magreth Magoma, Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Kimataifa cha Usuluhishi Tanzania (TIAC) akitoa ufafanuzi kwa waandishi wa habari kuhusu mafunzo na kongamano la ushirikishwaji wa wanawake kwenye utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala yaliyofanyika Jijini Dar es Salaam.*



*Watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Kituo cha Kimataifa cha Usuluhishi Tanzania (TIAC) wakimsikiliza ndugu Godson Nyange (hayupo pichani) Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Kituo cha Kimataifa cha Usuluhishi Tanzania wakati akiongea na waandishi wa habari kuhusu mafunzo na kongamano la ushirikishwaji wa wanawake kwenye utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala yaliyofanyika Jijini Dar es Salaam.*

# Dira, Dhima na Maadili ya Msingi

## Dira

**Kuwa Ofisi Mahiri ya Umma ya kusimamia mashauri ya madai na usuluhishi yanayoihusu Serikali**

## Dhima

**Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imedhamiria kusimamia na kuendesha mashauri ya Serikali kwa ufanisi na weledi wa hali ya juu**

# Maadili ya Msingi

1. Weledi
2. Uaminifu
3. Uwajibikaji
4. Uadilifu na Uhuru



osgtanzania osgtanzania osgtanzania